

TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA



TAARIFA KWA UMMA

MATOKEO YA USAILI – AJIRA MPYA MAHAKAMA

Dar es Salaam: 30/6/2022

Tume ya Utumishi wa Mahakama ilitangaza nafasi za ajira mpya kwa kada mbalimbali tarehe 02 Juni, 2022. Kufuatia tangazo hilo, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama anapenda kuwajulisha wale wote walioshiriki katika mchakato huo kwa hatua ya mwisho kuwa sasa mchakato huo umekamilika. Wale walioshinda usaili kwa nafasi mbalimbali watajulishwa kwa ujumbe kupitia simu zao za mkononi na barua pepe (email) zao.

Endapo ulishiriki mchakato huo na hukupata ujumbe wa simu wa kukujulisha na pia barua pepe yako (Uliyotumia wakati unaomba nafasi ya kazi), hadi kufikia **saa kumi jioni, Ijumaa tarehe 01 Julai, 2022** basi fahamu kuwa hujafanikiwa kwa awamu hii.

Kwa wale watakaopata ujumbe kwenye simu zao au barua pepe, utakuwa umetoka 'MAHAKAMA' na kwamba ni ujumbe kutoka kwenye mfumo wetu, kwa hiyo hawataweza kujibu bali watutumie uthibitisho wao kwenye barua pepe ya; maulizo.ajira@jsc.go.tz na kwenye subject andika 'KUKUBALI AJIRA.....' weka jina la kada uliyopata ajira yake. Majibu hayo ya uthibitisho yapatikane kufikia **Jumatatu tarehe 04/07/2022 saa tisa alasiri**.

Kwa maulizo ya saa 24; Email: maulizo.ajira@jsc.go.tz, simu **0734-219821**. Ukipata mawasiliano yetu ya simu ya mkononi, hakikisha ni kwa namba hii.

Imetolewa na;-

A handwritten signature in blue ink that reads 'Lydia Churi'.

Lydia Churi

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano
TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA**